

Swahili

# Karibu katika asili ya Norwei

Haki ya Ufikiaji wa Umma inampa kila mtu uhuru wa kutembelea asili ya Norwei.

Haki hii inaruhusu shamba ambalo halijalimwa na kwa kila mtu, haijalishi asili, jinsia au umri wako. Shamba ambalo halijalimwa ni misitu, milima, fuo, mabwawa na vingine kama hivyo

Hakikisha kwamba huharibu asili, wanyama wala mimea. Heshimu masilahi ya wamiliki wa mashamba na watu wengine.

Haki ya Ufikiaji haitumiki kernyr shamba lililolimwa kama bustani, shamba la mazao au sawa na hilo.



# Haki ya Kutembea inakuruhusu:

- kutembea katika msitu, milima na kandokando ya ufuo
- kuendesha baiskeli katika milima na kwenye njia
- kuogelea katika bahari, maziwa na mito
- kuteleza juu ya theluji na nje ya njia za skii
- kusanya beri na uyoga
- kuenda kuvua samaki katika bahari – watoto chini ya miaka 16 wanaweza kwenda kuvua katika maziwa na mito kuanzia 1/1 hadi 20/8 bila malipo. Kila mtu anastahili kununua leseni
- kuweka hema kwa siku na usiku mara 2 kwenye eneo moja – lazima liwe angalau mita 150 kutoka kwenye nyumba za wenyeji au dambra

## Tafadhali kumbuka:

- kupeleka takataka zako nyumbani
- usiwasumbue ndege na wanyama wa porini
- fungua malango kila mara na uheshimu wanyama wa kufugwa

Hizi ndizo sheria zilizorahisishwa katika haki ya Umma ya ufikiaji nchini Norwei. Soma zaidi hapa:

<https://www.miljodirektoratet.no/for-private/friluftsliv-og-allemannsretten>



Friluftsrådenes Landsforbund